

عليه السلام

الإمام الحسين

و تأصيل حقوق الإنسان

IMAM HUSAIN (A.S.)

NA UWEKAJI MSINGI WA HAKI ZA BINADAMU

Kimeandikwa na:
Sheikh Dkt. Abdullah Ahmad Yusuf

Kimetarjumiwa na:
Ustadh Amiri Mussa Kea

**IMAM HUSAIN (A.S.)
NA UWEKAJI
MSINGI WA
HAKI ZA BINADAMU**

الإمام الحسين عليه السلام وتأصيل
حقوق الإنسان

**Kimeandikwa na:
Sheikh Dkt. Abdullah Ahmad Yusuf**

**Kimetarjumiwa na:
Ustadh Amiri Mussa Kea**

ترجمة

الإمام الحسين عليه السلام وتأصيل
حقوق الإنسان

تأليف

عبد الله أحمد يوسف

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 – 9987 – 17 – 106 – 4

Kimeandikwa na:
Sheikh Dr. Abdullah Ahmad Yusuf

Kimetarjumiwa na:
Ustadh Amiri Mussa Kea

Kimehaririwa na:
Ustadh Haj. Hemedi Lubumba Selemani

Kimesomwa Prufu na:
Al-Haj. Ramadhani S. K. Shemahimbo

Kimepitiwa na:
Al-Haj. Mujahid Rashid

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Septemba, 2018
Nakala: 2,000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Al-Itrah Foundation

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640 / 2127555

Barua Pepe: alitrach@yahoo.com

Tovuti: www.alitrach.info

Vitabu mtandaoni: www.alitrach.info/ebooks/

ILI KUSOMA QUR'ANI MUBASHARA
KWA NJIA YA MTANDAO
TEMBELEA www.somaquran.com

YALIYOMO

Dibaji.....	5
Neno la Mchapishaji.....	6
Utangulizi.....	9
Imam Husein <small>عليه السلام</small> na uwekaji msingi wa Haki za Binadamu.....	13
1. Kulinda utukufu wa Binadamu:.....	13
2. Kufaidika na uhuru:.....	16
3. Usawa baina ya watu:.....	18
4. Haki ya kuchagua kiongozi:.....	22
Vipi tunawajibika katika Kuamiliiana na suala la Haki za Binadamu.....	24
1. Kukuza Utamaduni wa kutetea Haki:.....	24
2. Kutafuta Haki zilizowekewa Azimio:.....	26
3. Kuheshimu Haki za watu:.....	27
Hitimisho la Miski.....	29
Rejea.....	30

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

DIBAJI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenye kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam

Al Itrah Foundation

Barua Pepe: alitrh@yahoo.com

SMS: +255 778 300 140

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako kimetarjumiwa kutoka lugha ya Kiarabu kwa jina la, *al-Imam al-Husain 'Alayhi 's-Salam wa Ta'sil Huquqa 'l-Insan*, kilichoandikwa na Sheikh Dkt. Abdullah Ahmad Yusuf. Sisi tumekiita, *Imam Husain (a.s.) na Uwekaji Msingi wa Haki za Binadamu*.

Imam Husain (a.s) ni mjukuu wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kutokana na binti yake mpenzi Fatma Zahra (a.s.), na baba yake ni Imam Ali bin Abu Talib (a.s.). Ni Imamu wa tatu katika Maimamu Thenashara wa Ahul Bayt (a.s.).

Imam Husain (a.s.) ni maarufu sana kutokana na muhanga alioutoa hapo Karbala mwaka wa 60 Hijria. Na kila mwaka unapofika mwezi wa Muharram, Waislamu kote ulimwenguni hufanya majlisi za kukumbuka masaibu ya Karbala yaliyomfika mjukuu huyu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Imam Husain alifanya mageuzi makubwa na ya kihistoria katika ubinadamu, wala si kwa Waislamu tu bali kwa wanadamu wote - kama utakavyoona katika kitabu hiki.

Kama ilivyo kawaida Maimamu hawa wanaotokana na Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ni wateule wa Mwenyezi Mungu, maisha yao ni mfano wa kuigwa katika jamii ya wakati ule na wakati huu na wakati ujao.

Mwandishi katika kitabu hiki pamoja na mambo mengine anaelezea jinsi Imam Husain (a.s.) alivyo-weza kuleta mageuzi na mabadiliko katika jamii ya wanadamu.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Sheikh Amiri Mussa kwa kazi kubwa aliyofanya ya kukitarjumi kitabu hiki kutoka lugha yake ya asili ya Kiarabu kuja katika lugha ya Kiswahili. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah Mwenye

kujazi awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

Mchapishaji

Al-Itrah Foundation

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

UTANGULIZI

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemtukuza binadamu, na akamfanya yeye ni mwenye kufadhilishwa juu ya viumbe wengine, anasema (s.w.t):

وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِنَ
الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى كَثِيرٍ مِمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا

“Hakika tumewatukuza wanaadamu na tumewabeba nchi kavu na baharini na tumewaruzuku vitu vizuri na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tuliowaumba.”¹

Na hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemtukuza mwanadamu huyo kwa kumpa akili, riziki na uwezo wa kusafiri nchi kavu na baharini, yote hayo ili aishi hali akiwa huru mwenye utukufu.

Na utukuzwaji mkubwa wa binadamu sio mwingine nao ni kuhifadhi na kulinda utukufu wake wa ubinadamu, kulinda haki za kimaada (kimwili) na kiroho, na uharamu wa kujitwalia haki hiyo au

¹ Qur’ani Tukufu Sura Bani Israil; 17:70.

kuiondoa yaani haki miongoni mwa haki zake za msingi zilizowekwa na kuazimiwa, aidha kujiepusha kwa aina yoyote ile ambayo kwa njia moja au nyingine itahatarisha na kuvunja haki za binadamu wengine.

Uislamu haukutosheka tu kwa wosia na mafundisho ya kidini ambayo huhimiza juu ya wajibu wa kumheshimu mwanadamu na kulinda haki zake, bali zimeanzishwa jumuiya nyingi zenye kujishughulisha na masuala ya utetezi wa haki za binadamu, wajibu wa kumpa yeye haki zote za msingi kwa upande mmoja, na uharamu wa kupituka mipaka yake au kupitiliza juu ya haki miongoni mwa haki kwa upande mwingine.

Na katika Qur'ani tukufu inakadiriwa kuwepo kwa aya za Qur'ani 200 ambazo zinatoa ishara juu ya haki za binadamu katika Uislamu, ambazo zinavuka haki mia moja, na wakati tangazo la ulimwengu lilipotolewa kuhusiana na haki za binadamu ambazo azimio lilitolewa na kupitishwa na jumuiya zote za umoja wa mataifa terehe 10/12/1948 A.D zipo mada 29 zilizoandikwa kuhusiana na haki za msingi za binadamu.

Ama katika Sunna ya Mtume ﷺ pamoja na maneno ya Maimamu wa Ahlul-Bayt watoharifu, hakika yamekuwepo maandiko na hadithi mbalimbali kuhusiana na haki za binadamu kwa kiwango

kikubwa. Kwa hakika imepokewa kutoka kwa Mtume ﷺ amesema: “Mwislamu kwa Mwislamu mwenzake ni haramu damu yake, mali yake na kumvunjia heshima yake.”²

Na andiko hilo linatoa ishara tosha kwamba ni lazima kuheshimu haki za binadamu za kimaada kama vile; mwili wake na mali yake, pia kuheshimu haki zake za kiroho kwa mfano; utukufu wake, uhuru wake na fikra zake.

Na ili binadamu aweze kufaidika na haki zake basi hapana budi kuwepo utaratibu na mpango kabambe wenye kusimama imara juu ya uadilifu na ulinganifu wa kijamii. Na hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameamrisha uadilifu katika hukumu na amekataza dhulma. Basi zipo ndani ya Qur’ani tukufu Aya zipatazo 54 juu ya suala la uadilifu ambazo zimegawanyika katika maneno matatu; adli, *Qistwi* na *Qistwaas*.

Na kwamba Mola Muumba amekataza dhulma, na zipo Aya zipatazo 320 ambazo amewaahidi madhalimu adhabu. Na kati ya Aya hizo zipo zenye kutoa ishara mbalimbali kwamba dhalimu ni mwenye kutelekezwa na asiye na thamani yoyote ile mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w.t), aidha ni mwenye kuchu-

² *Muniyatul-Muriid*, uk. 327 cha Shadidi Thaani na *Sahihi Muslim*, uk. 968, hadithi na. 6541.

kiwa, na matokeo yake ni kuishi maisha mabaya duniani na akhera.

Kitabu hiki kinajadili na kudadavua kwa muhtasari asili (chimbuko) ya haki za binadamu kwa mujibu wa maneno, hotuba na kauli mbiu za Imam Husein عليه السلام siku ya Ashura katika uwanja wa Karbala, ambazo zinatilia mkazo juu ya haki za msingi za binadamu kwa kuzingatia kuwa huo ni mhimili wa utukufu wa binadamu, na kudhamini haki zake na uhuru wake wa msingi.

Na hatimaye ... ninamuomba Mwenyezi Mungu (s.w.t) ajaalie kitabu hiki uzito katika mzani wa amali zangu, na kininufaishe mimi huko akhera, Qur'ani tukufu inasema:

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ مَالٌ وَلَا بَنُونَ إِلَّا مَنْ أَتَى اللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ

“Siku ambayo haitafaa mali wala wana. Isipokuwa mwenye kuja kwa Mwenyezi Mungu na moyo uliosalimika.” (Qur'ani Tukufu Sura ash-Shu'araa 26:88-89)

Hakika yeye – (s.w.t) – Ndiye fikio la marejeo, na lengo la matumaini pia chimbuko la rehema, majazo mema na utoaji. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuombwa msaada.

Abdullah Ahmad Yusuf

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

IMAM HUSEIN عليه السلام NA UWEKAJI MSINGI WA HAKI ZA BINADAMU

Tunapozingatia kwa makini maneno, hotuba na kauli mbiu za Imam Husein عليه السلام siku ya Ashura katika uwanja wa Karbalaa tunakuta kwamba zimejikita juu ya misingi ya haki za binadamu. Kwa hakika haki hizo zimekuwa ni mhimili wa utukufu wa binadamu, dhamana ya haki zake na uhuru wake wa kimsingi.

Na miongoni mwa haki za msingi zaidi ambazo Imam Husein عليه السلام amezitolea ishara katika hotuba zake na maneno yake, hapa tunazielezea kama ifuatavyo:

1. Kulinda utukufu wa Binadamu:

Hakika miongoni mwa haki za msingi mno za binadamu ni kulinda utukufu wa binadamu na kutouchezea, kupituka mipaka yake au kuuponda, sawa iwe kwa vitendo au kwa maneno.

Na tunapochunguza tangazo na azimio la mkataba la ulimwengu juu ya haki za binadamu, hakika sisi tunakuta zimetolewa ishara katika dibaji yake kukiri na kutambua utukufu wenye kuweka msingi katika jengo la binadamu, na haki zao zenye kukubalika

zilizothibiti. Kwa mfano; msingi wa uhuru, uadilifu na amani, kwa hakika kila mtu anataka aneemeke hapa ulimwenguni kama vile wanadamu wengine wanavyoneemeka. Awe na uhuru wa kusema na wa kutoa maoni, na awe huru kutokana na hofu na mahitajio. Kwa hakika ni jambo la dharura kuwepo kanuni ambayo hutetea haki za binadamu ili isifikie hali ya uasi kutokana na ugandamizaji na dhuluma.

Na dibaji ikaongeza tangazo la ulimwengu juu ya haki za binadamu kwamba watu wa umoja wa mataifa wametilia mkazo katika azimio la umoja wa mataifa ambalo lilisainiwa tarehe 26/6/1945 A.D, utetezi wa haki za msingi za mwanadamu, utukufu wa mtu na thamani pamoja na hadhi yake, ni kwamba watu wote wanaume na wanawake wana haki sawa, na kuimarisha jambo lake juu ya kupiga hatua mbele katika maendeleo ya kijamii, pia kuinua kiwango cha maisha katika kivuli cha uhuru uliokamilika. Hakika mataifa wanachama yamekata shauri na kuahidi kwamba yatasaidiana pamoja na Umoja wa Mataifa ili kuheshimu haki za binadamu na uhuru wake wa msingi.

Kisha linaeleza andiko la kwanza katika tangazo la kwamba hakika watu wanazaliwa wakiwa sawa katika utukufu na haki. Wamepewa akili na dhamira, hivyo ni juu yao waamiliane wao kwa wao kwa roho ya undugu, kama vile inavyotaja mada ya pili; kila binadamu afurahie haki na uhuru unaopatikana

katika tangazo la azimio bila ubaguzi, hususan kijinsia, rangi, lugha, dini, maoni ya kisiasa, maoni yoyote yale, uzalendo, masuala ya kijamii, utajiri, kuzaliwa au jambo lolote lile.

Kwa hakika Imam Husein عليه السلام ametilia mkazo na kujikita katika mchakato wa mageuzi yake ya kuleta mabadiliko na kuweka mambo sawa juu ya kulinda na kuhifadhi utukufu wa binadamu, kukataa utumwa, na kupendelea kufa kuliko kuishi katika udhalili na utwana na pia kuvunjiwa heshima, hadhi na utu, anasema عليه السلام: “Hakika mdanganyifu na mtoto wa mdanganyifu, amejikita baina ya mambo mawili; upanga na udhalili, na sisi tuko mbali na udhalili, Mwenyezi Mungu analikataa hilo kwetu, kwa Mtume Wake na waumini, na mazazi yetu yamekuwa mazuri na yametoharika, pia yenye munkari, na nafsi zilizokataa kutii watu waovu na mapambano ya watukufu.”³

Basi Imam Husein عليه السلام alikataa kuishi katika hali ya kuwanyenyekea madhalimu na kukosa kufaidika na uhuru wa binadamu ambao Mwenyezi Mungu (s.w.t) amempatia binadamu, na akaamua kuchagua njia ya kufa shahidi kwa ajili ya kulinda utukufu wa binadamu, aidha kufanya hali ya umma kuwa nzuri,

³ *Luhuuufu fi Qatliy Tufuuf*, uk. 59 cha Sayyid ibn Twaus Huseiny, kimechapishwa na Muhri, Qum – Iran, chapa ya kwanza mwaka 1417 A.H.

kama alivyosema ﷺ: “Hakika mimi sikutoka ili kufanya shari, wala kutaka ukubwa, wala kufanya ufisadi wala kudhulumu, bali hakika nimetoka ili kutengeneza yale yaliyoharibika katika umma wa babu yangu, ninataka niamrishe mema na nikataze maovu.”⁴

Imam Husein ﷺ mahali pengine amesema: “Hapana.... naapa kwa Mwenyezi Mungu, sitatoa mkono wangu utoaji wa dhalili, wala sitokimbia ukimbaji wa mtumwa.”⁵

Kwa hivyo Imam Husein ﷺ alichagua kifo kwa kupata utukufu kuliko kuishi maisha ya udhalili na fedheha hali kadhalika kukosa utu, hadhi na heshima, kwani binadamu asipolinda utu wake atapoteza thamani ya ubinadamu wake.

2. Kufaidika na Uhuru:

Uhuru upo wa aina mbili; uhuru wa ujumla na uhuru mahsusi, na huu ni muhimu zaidi katika haki za binadamu, na katika haki hii inaingia; haki ya kuamini na kuitakidi, na haki ya kutoa maoni na kusema.

⁴ *Biharul-Anwar*, Juz. 44, uk. 329 cha Allama Majlisi, *Kitabul-Futuuh*, Juz. 5, uk. 33 cha Ahmad bin A'tham Kuufi, kimechapishwa na Darul-Nadwat Jadida Beirut.

⁵ *Irshad*, uk. 363 cha Sheikh Mufiid.

Hakika Uislamu umeutukuza uhuru, na kuuzingatia kuwa ni miongoni mwa mihimili muhimu zaidi ya ubinadamu moja kwa moja. Kwa hakika hiyo ni miongoni mwa haki kubwa zaidi za mwanadamu na hiyo ni haki yake, kwa hivyo binadamu anahitajika kutumia kikamilifu haki yake hiyo, kama Mwenyezi Mungu (s.w.t) alivyotaka hivyo, Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

“... وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِمْ ...”

“Na kuwaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao.”⁶

Na Imam Ali عليه السلام anasema: “Usiwe mtumwa wa mwingine, hakika Mwenyezi Mungu amekuumba wewe huru.”⁷

Na msingi wa ujumla katika Uislamu ni kwamba yeyote hana madaraka ya kumtawala mwingine isipokuwa yule aliyeelezwa na dalili inayozingatiwa kisharia.

Na Imam Husein عليه السلام ametolea ishara katika wajibu wa kufaidika na uhuru husika, bali akawaomba maadui zake waishi huru katika dunia yao, aliwaambia: “Ikiwa hamna dini, na hamuogopi siku ya mwisho, basi kuweni huru katika dunia yenu.”⁸

⁶ Qur’ani Tukufu Sura al-A’araf 7:157.

⁷ *Miizanul-Hikma*, Juz. 1, uk. 582.

⁸ *Biharul-Anwar*, Juz. 45, uk. 51 cha Allamah Majlisi.

Na andiko hili la Imam Husein عليه السلام linatoa ishara katika kutilia mkazo juu ya thamani ya uhuru. Kwa hivyo binadamu ni mtu huru na lazima aishi huru hapa duniani hata kama hana dini, hakika uhuru unatafutwa hauji wenyewe, na binadamu anapaswa kutambua thamani ya ubinadamu wake.

Imam Husein عليه السلام amesema: “Sioni kifo isipokuwa ni wema, na kuishi na madhalimu ni fedheha.”⁹ Basi kifo katika utukufu, uhuru na heshima ni bora kuliko kuishi katika udhalili, fedheha pamoja na madhalimu. Hakika binadamu haiwezekani ahisi wema na utukufu hali ya kuwa yeye anaishi katika kivuli cha dhuluma, ugandamizwaji na udikteta, kwa hivyo Imam عليه السلام alipendelea kufa akiwa mtukufu kuliko kuishi katika udhalili, na fedheha chini ya watawala madhalimu.

3. Usawa baina ya watu:

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewaumba watu wote kutokana na udongo, anasema:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ إِذَا أَنْتُمْ بَشَرٌ تَنْتَشِرُونَ

“Na katika Ishara Zake ni kuwa amewaumba kwa udongo; kisha mmekuwa watu mnaoenea.”¹⁰

⁹ *Manaqib Aali Abi Talib*, Juz. 4, uk. 76 cha Ibn Shahr Ashuub.

¹⁰ Qur’ani Tukufu Sura ar-Rum; 30:20.

Na kwa hivyo hakuna ubora na fadhila juu ya mwarabu kwa asiyekuwa mwarabu, wala mweupe kwa mweusi isipokuwa kwa uchamungu na amali njema. Na Qur’ani tukufu inakariri katika sehemu mbalimbali kwamba jinsi ya wanadamu wote wameumbwa kutokana na udongo na nafsi moja, anasema (s.w.t):

”يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ
وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً.....“

“Enyi watu! Mcheni Mola wenu ambaye amewaumba kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe katika nafsi hiyo, na akaeneza kutokana na hao wawili wanau-me wengi na wanawake.....”¹¹

Basi watu ni sawa sawa katika asili na maumbile, mwanzo na asili, na hakika Bwana Mtume ﷺ ametilia mkazo suala hilo kwa kauli yake: “Watu ni sawa sawa kama vile meno ya chanuo.”¹²

Uislamu unakataza kuwabagua watu kwa misingi ya rangi, utaiifa, jinsia, umadhehebu au aina yoyote ile ya ubaguzi baina ya watu, wote wameumbwa na Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutokana na nafsi moja na kutokana na udongo.

¹¹ Qur’ani Tukufu Sura an-Nisaa’; 4:1.

¹² *Biharul-Anwar*, Juz. 75, uk. 251 cha Allamah Majlisi, hadith ya. 99.

Na usawa miongoni mwa watu – ambao unahe-sabiwa ni miongoni mwa yale ambayo yanatengeza na kuweka msingi wa jengo la uadilifu katika jamii – inaamanisha kwamba usawa mbele ya sheria na kanuni, usawa katika utumiaji wa fursa, usawa katika kushika madaraka na utumishi wa umma, usawa katika kutafuta chumo (riziki) na vipaumbele, na usawa katika haki na wajibu mbalimbali.

Na yale yote yanayozikumba jamii mbalimbali katika ulimwengu huu wa leo kutokana na matatizo ya muda mrefu hurejea – katika kiungo miongoni mwake – hadi kuenea katika maisha ya wote, na kukosekana utekelezaji wa kifursa kati ya watu, na upambanuzi juu ya misingi tofauti, kwa yale ambayo yanapelekea kurudisha umma nyuma na kuufanya ukose maendeleo, pia kutokuwepo uadilifu katika jamii.

Basi usawa – una maana kwamba – ni kukataa ubaguzi juu ya msingi wa uzawa, utaiifa, umadhehebu na yanayofanana na hayo. Basi uzawa, lugha, ukabila na utaiifa vyote hivyo vinaingia ndani ya umoja wa asili ya binadamu ambapo Qur’ani tukufu imelielezea hilo katika kauli yake (s.w.t) anasema:

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا
وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ
خَبِيرٌ

“Enyi watu! Hakika Sisi tumewaumba kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumewafanya mataifa na makabila ili mjuane. Hakika mtukufu zaidi yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni aliye na takua zaidi yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye habari.”¹³

Basi kujifaharisha na kujiona bora kwa hakika kigezo kiwe ni uchamungu, na sio nasaba, uzawa, ukabila au yale yote yanayofanana na hayo katika maumbile miongoni mwa wanadamu.

Na tunakuta katika sira ya Imam Husein عليه السلام siku ya ashura katika uwanja wa Karbalaa amejikita juu ya thamani na utukufu wa binadamu pale ambapo aliweka shavu lake tukufu juu ya shavu la John, mtumwa mweusi ambaye alikuwa ni mtwana wa Abu Dharri Ghaffari, na juu ya shavu la kijana mturuki Wadhih bin Aslam. Vivyo hivyo alifanya kwa kipenzi cha moyo wake Ali Akbar ambaye alikuwa mzuri mno, nayo ni ishara ya ukamilifu ambao unatilia mkazo juu ya thamani ya usawa miongoni mwa watu kwa kuangalia upande wa ubinadamu, na hilo linalazimu kufaidika kwalo katika utukuzaji wa thamani ya ubinadamu uliotokana na mapinduzi ya Imam Husein عليه السلام.

¹³ Qur’ani Tukufu Sura al-Hujurat; 49:13.

4. Haki ya kuchagua Kiongozi:

Uhuru wa kisiasa huhesabiwa ni sehemu muhimu miongoni mwa viungo vya uhuru wa binadamu. Na kwa ibara nyingine uhuru wa kisiasa ni tawi la asili ya yote, na ndiyo asili ya uhuru wa binadamu.

Na haki za uhuru wa kisiasa ni nyingi, kati ya hizo ni haki ya kuchagua kiongozi mwadilifu, na kumkataa kiongozi dhalimu, kwani Uislamu umeamrisha uadilifu na umeharamisha dhulma, na kauli mbiu yake: Usawa katika haki na wajibu mbalimbali, katika kutumia fursa, na kuthibitisha uadilifu katika jamii. Na hakika Imam Husein عليه السلام aliitendea kazi haki yake ya kisheria pale alipokataa kumpa kiapo cha utii kiongozi dhalimu alisema: “Hakika sisi ni Ahlul-Bayt wa Mtume, ni asili ya ujumbe, sehemu ya mapishano ya Malaika, kwetu sisi Mwenyezi Mungu ameanzisha na kwetu sisi Mwenyezi Mungu amehitimisha, na Yazid ni mtu movu, mnywaji pombe, muuaji wa nafsi iliyoharamishwa, ni mfanyaji ufasiki, maovu na ufuska wazi wazi, na mfano wangu hambai mfano wake, lakini tunaamka na mnaamka, tunaangalia na mnaangalia, sisi ndiyo wenye haki zaidi kupewa kiapo cha utii na ukhalifa.”¹⁴

¹⁴ *Biharul-Anwar*, Juz. 44, uk. 325 cha Allamah Majlisi.

Basi Imam Husein ؑ anastahiki zaidi kuwa khalifa na sio mwingine, naye hawezi daima kumbai kiongozi anayevunja haki, makubaliano na ahadi, aliyesimama kufanya dhuluma kwa upande mmoja na kuwafanya watu watumwa kwa upande mwingine. Hakika Imam Husein ؑ aliweka uhai wake kuwa ni thamani katika kuithibitisha haki, na kuitokomeza batili, amesema ؑ: “Je, hamuoni haki haitendewi kazi na batili haikatazwi, basi muumini apende kukutana na Mwenyezi Mungu akiwa mwenye haki.”¹⁵

Na kwa sababu hii – na nyinginezo – Imam Husein ؑ akafanya mapinduzi, na akakataa dhuluma ya Yazid na serikali yake, akasema: “Na mfano wangu mimi hambai mfano wake.”¹⁶

Na hilo limebainishwa na Imam Husein ؑ kwamba ni haki ya umma kuchagua kiongozi mwadilifu ambaye anatekeleza amri za Mwenyezi Mungu (s.w.t), anasimamisha uadilifu na anazuia dhuluma. Ama kiongozi dhalimu ambaye anadhu-

¹⁵ *Tuhaful-Uquul*, uk. 245 cha Ibn Shu’bat Harrani, kimechapishwa na Taasisi Tashru Islamiy lil-Jama’at Mudarrisiina, Qum - Iran chapa ya pili mwaka 1404 Hijiria. na Lahuuf Fil Qatli Tufuuf uk. 71 cha Sayyid Ibn Tausi Huseiny, kimechapishwa na Muhri – Qum - Iran, chapa ya kwanza mwaka 1417 Hijiria.

¹⁶ *Biharul-Anwar*, Juz. 44, uk. 325.

lumu na kutesa watu, anavunja haki za binadamu, anahukumu kwa dhuluma, ubabe, kidikteta na asiyefuata kanuni, huyo wala hakuna baia kwake, na hakika Imam Husein ؑ ameliweka wazi hilo kivitendo kwa kukataa kumbai Yazid, na kwa hivyo haifai kumbai mfano wake.

VIPI TUNAWAJIBIKA KATIKA KUAMILIANA NA SUALA LA HAKI ZA BINADAMU

Baada ya kujua yale yaliyoletwa na mapinduzi ya Imam Husein ؑ kutokana na kujali na kutilia muhimu suala la thamani na mafundisho ya haki za binadamu, ni juu yetu tutupie macho sira ya Imam Husein ؑ siku ya Ashura na siku za kabla yake huko Karbalaa na, majukumu yetu na wajibu wetu ni kama vile watu wengine pamoja na jamii mbalimbali kuelekea suala la haki za binadamu, nayafupisha katika maneno yafuatayo:

1. Kukuza Utamaduni wa kutetea Haki:

Miongoni mwa mambo yenye umuhimu mkubwa, yatupasa sisi kurejea mikataba, matangazo, maazimio na sheria za kitaifa na za kimataifa ambazo zimekubali suala la haki za binadamu, kwa namna ambayo yanakuza utamaduni wa haki kwa watu na

jamii mbalimbali. Na yale yaliyo muhimu zaidi yaliyotolewa kutoka katika vyanzo vyenye kuamini na kukubalika kuhusiana na suala la haki za binadamu, na vyombo vya habari vya ulimwengu juu ya haki za binadamu, azimio lake liliwekwa na jumuiya za Umoja wa Mataifa terehe 10/12/1948 A.D, na tangazo hili lilikuwa limepata kanuni zake kutoka katika matangazo yaliyotangulia, kuanzia pale yalipotokea mapinduzi ya kifaransa mwaka 1789 A.D, ambapo ulitangazwa mkataba wa haki za binadamu kwa kuzingatia kuwa hizo ni haki za msingi kwa kila mtu, kisha zikapitishwa na katiba za mataifa yote, mpaka zikawa nchi zote wanachama wa umoja wa mataifa zikaandika haki za binadamu katika katiba zao, hata kama baadhi yake hazitekelezi haki hizo kivitendo.

Na kwa usomaji wa tangazo la ulimwengu mzima juu ya haki za binadamu inakuwa wazi kwamba misingi ya ujumla ambayo imepatikana katika ugawaji wa haki na uhuru iliyotangazwa katika tangazo lake ni kama ifuatavyo:

Mosi: Haki ya uhuru wa miji.

Pili: Haki ya uhuru wa kisiasa.

Tatu: Haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni.

Mwanadamu anahitaji kuukuza uelewa wa utamaduni wake kuhusu haki kwa kupitia na kusoma mikataba, matangazo na maazimio mbalimbali

ambayo huelezea suala la haki za binadamu, kama vile ni muhimu kusoma baadhi ya vitabu ambavyo vimeandikwa na wasomi na wanazuoni kuhusiana na suala la haki za binadamu ili kujua rai na maoni ya kisheria katika kuzielekea hizo, pia kujua dalili juu ya wajibu wa kuheshimu haki hizo kutoka katika Kitabu, Sunna, ijimai na akili.

Na haki za binadamu zimekusanywa katika vipengele vitano vya msingi navyo ni: Uadilifu, maadili, uhuru, haki, na wajibu, ni jambo la dharura kugusia haki hizo kwa ujumla – lau kwa uchache – mpaka mwanadamu ajue haki zake na yale yanayomwajibikia juu yake.

2. Kutafuta Haki zilizowekewa Azimio:

Uislamu umezingatia (haki za binadamu) ni miongoni mwa suala la dharura la kibinadamu, maisha ya binadamu hayawezi yakawa bila ya haki hiyo, na huko haifai kwa yeyote kujitwalia haki hiyo, kama vile haifai kwa mtu yeyote yule aiache haki yake ya msingi. Kwani katika kuiacha binadamu atapoteza ubinadamu wake, atapata hasara na kupoteza utukufu wake kama vile yule mwelewa na mpambanuzi wa mambo. Kwa hivyo ni juu ya mwanadamu pale zinapovunjwa haki zake za msingi basi azitafute hizo kwa udi na uvumba, na kama si hivyo basi anyamaze, vivyo hivyo haki za kijamii, kabla

binadamu hajatafuta haki zake ni juu yake azijue haki hizo kwanza, na namna ya kuzipata, kama ikiwa hazijui haki zake basi hawezi kutafuta kile ambacho asichokijua. Kwa mantiki hiyo hakika utafutaji haki za msingi unakuja katika hatua ya pili baada ya kutanguliwa na ukuaji juu ya utamaduni wa kuelewa haki ambao tumeutolea ishara hapo kabla.

3. Kuheshimu Haki za watu:

Uvunjaji wa haki za binadamu zilizowekwa kuna wakati uvunjaji huo unatoka kwa sultani anayehukumu na kutawala mji huu au ule, na mara nyingine unatoka kwa watu kuelekeana wao kwa wao. Na hili ndilo tunataka kulitolea ishara hapa. Hakika kuheshimu haki za watu ni amri ya kisheria na kiakili, haifai kuzivunja kisheria kwa vyoyote vile itakavyokuwa, bali ni wajibu kuheshimu haki na kutekeleza wajibu mbalimbali. Hali kadhalika haifai mtawala wa mji wowote ule kuvunja haki za watu, vivyo hivyo haifai watu wao kwa wao kuvunjiana haki zao, kwa njia ya kuwatawala au kuwa na mamlaka juu ya wengine, kupora mali zao, kuondoa heshima zao na kuponda utu wao wa kidini au wa kitamaduni.

Ni wajibu watu kuheshimiana wao kwa wao, wasaidiane katika mambo mema na uchamungu. Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

”...وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ
وَالْعُدْوَانِ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ“

“Na saidianeni katika wema na takua wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.”¹⁷

Pia Qur’ani tukufu inazungumzia lengo la kuumbwa watu mataifa na makabila mbambali, nalo si lingine, bali wanadamu wapate kujuana, Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

”يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا
وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ.....“

“Enyi watu! Hakika Sisi tumewaumba kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumewafanya mataifa na makabila ili mjuane. Hakika mtukufu zaidi yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni aliye na takua zaidi yenu.....”¹⁸

Na uwepo wa tofauti katika dini, madhehebu, uzawa, ukabila sio kitu ambacho kinasababisha kuwepo uvunjaji wa haki za binadamu, bali inawajibika watu

¹⁷ Qur’ani Tukufu Sura al-Maida; 5:2.

¹⁸ Qur’ani Tukufu Sura al-Hujurat; 49:13.

wote kuwa sawa mbele ya sheria, bila kuwepo tofauti kati ya mweupe na mweusi, wala kati ya mwarabu na asiyekuwa mwarabu, hakika kigezo cha ubora fadhila ni uchajimungu na elimu.

HITIMISHO LA MISKI

Hakika mapinduzi ya Imam Husein عليه السلام ambayo yalikuwa ni kwa ajili ya kuweka uadilifu, na kukataa dhuluma, hakika yalianzisha msingi wa kuheshimu haki za binadamu, na mapinduzi haya yakawa ni chuo cha kufundisha na kukuza utamaduni wa kutetea haki kulingana na mafunzo na misingi ya Kiislamu na hukmu zake.

Na miongoni mwa malengo ya mapinduzi ya Imam Husein عليه السلام ni kumtengeneza mwanadamu awe mfuataji na mwenye kushikamana na mafunzo ya mitume, misingi ya kidini, haki za binadamu na maadili mema ya Kiislamu.

Na pia miongoni mwa malengo ya mapinduzi hayo ni wajibu wa kufanya kazi katika kuweka na kueneza uadilifu katika jamii, pia kusimama kidete dhidi ya dhuluma, na kukabiliana na madhalimu, ambao wanavunja haki za binadamu na haki za watu, hali kadhalika haki za Mwenyezi Mungu.

Kwa hakika Imam Husein عليه السلام alisimama imara kwa ajili ya kutengeneza mambo yaliyoharibika, kuam-

risha mema na kukataza maovu, kuhuisha Sunna, na kuifisha bidaa. Aidha kusimama ngangari dhidi ya madhalimu, na kutendea kazi kulingana na hukmu za Mwenyezi Mungu (s.w.t) maishani, kufaidika na uhuru wa ujumla, na kuweka misingi ya uadilifu, haki, uhuru na amani, kuupa hadhi, utukufu wa ubinadamu, na kueneza akhlaq na maadili mema ya Kiislamu katika jamii.

REJEA

1. Qur'ani tukufu.
2. *Tuhaful- 'Uquul an Aali Rasuul*, cha Ibn Shu'bat Harrani, Abu Muhammad Hasan bin Ali bin Husein. Kimesambazwa na Taasisi ya Nashri Islami lil-Jama'at Mudarrisiina, Qum - Iran, chapa ya pili mwaka 1404 A.H.
3. *Manaqib Aali Abi Twalib* cha Ibn Shahr Ashuub, Abu Ja'far Muhammad bin Ali Saruway Mazandaraani aliyefariki 588 A.H, kimehakikiwa na kupangwa na Dr. Yusuf Buqai, kimechapishwa na Darul-Adhwai, Beirut – Lebanon, chapa ya pili mwaka 1412 A.H – 1991 A.D.
4. *Luhuuf fi Qatli Tufuut* cha Ibn Tausi, Abu Qasim Ali bin Musa bin Ja'far bin Muhammad, aliyefariki 664 A.H, kimechapishwa na Muhr, Qum – Iran, chapa ya kwanza 1417 A.H.

5. *Miizanul-Hikma* cha Ray Shahri, Muhammad, kimechapishwa na Taasisi ya Darul-Hadiith Thaqafiyyat, Beirut – Lebanon, chapa ya pili 1419 A.H.
6. *Sahih Muslim* cha Qashiiry Naysabuuri, Abu Husein Muslim bin Hajjaj bin Muslim. Amekufa 261 A.H. Kimechapishwa na Maktabat Misriyyat, Beirut, chapa ya mwaka 1423 A.H – 2002 A.D.
7. *Muniyatul-Muriid fi Adabil-Mufiid wal-Mustafiid* cha Aamili, Zayn Diin Bin Ali Jub'i, aliyekufa 965 A.H, Maarufu (Shahiid Thaani), kimechapishwa na Maktab I'lamul-Islamiy, Qum, chapa ya pili 1414 A.H.
8. *Kitabul-Futuuh Kuufi* cha Ahmad bin A'tham, kimechapishwa na Darul-Nadwat Jadiidat, Beirut, chapa ya kwanza, tarehe ya kuchapishwa kwake haikutolewa.
9. *Biharul-Anwar* cha Allamah Majlisi, Muhammad Baqir bin Muhammad Taqi, kimechapishwa na Muassasat Ahlul-Bayt, chapa ya nne mwaka 1409 A.H – 1989 A.D.
10. *Irshaad* cha Al-Mufiid, Abu Abdillah Muhammad bin Muhammad bin Nuuman 'Akbari Baghdadi (amekufa 413 A.H), kimechapishwa na Haydariyyat, Najaf – Iraq, chapa ya pili 1392 A.H – 1972 A.D.

IMAM HUSAIN (A.S.)

NA UWEKAJI MSINGI WA HAKI ZA BINADAMU

Mwenyezi Mungu amemtukuza binadamu, na akamfanya yeye ni mwenye kufadhilishwa juu ya viumbe wengine, kama anavyosema katika aya hii:

“Na hakika tumewatukuza wanadamu na tumewabeba nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku katika vitu vizuri, na tumewatukuza kuliko wengi wa wale tuliowaumba kwa utukufu mkubwa.” (17:70)

Kwa hakika hakika Mwenyezi Mungu (tabaraka wa ta'ala) amemtukuza mwanadamu kwa kumpa akili, riziki na uwezo wa kusafiri nchi kavu na baharini, yote hayo ili aweze kuishi akiwa kama mtu huru na mwenye utukufu.

Na utukuzwaji mkubwa wa binadamu sio mwingine ila ni kuhifadhi na kulinda utukufu wake wa ubinadamu, kulinda haki za kimaada (kimwili) na kiroho, na uharamu wa kujitwalia haki hiyo au kuiondoa miongoni mwa haki zake za msingi zilizowekwa na kuazimiwa, pamoja na kujiepusha kwa aina yoyote ile ambayo kwayo itahatarisha na kuvunja haki za binadamu.

Kitabu hiki kinajadili na kuchambua kwa muhtasari asili na chimbuko la haki za binadamu kwa mujibu wa maneno, hotuba na kauli mbiu za Imam Husain (a.s.) alizotoa siku ya Ashura katika uwanja wa Karbala ambazo zinatilia mkazo juu ya haki za msingi za binadamu kwa kuzingatia kuwa huo ni mhimili wa utukufu wa binadamu, haki zake na uhuru wake wa kimsingi.

Imam Husain alifanya mageuzi makubwa na ya kihistoria katika ubinadamu, wala si kwa Waislamu tu bali kwa wanadamu wote - kama utakavyoona katika kitabu hiki.

Kama ilivyo kawaida Maimamu hawa wanaotokana na Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ni wateule wa Mwenyezi Mungu, maisha yao ni mfano wa kuigwa katika jamii ya wakati ule na wakati huu na wakati ujao.

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Al-Itrah Foundation

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640 / 2127555

Barua Pepe: alitrah@yahoo.com

Tovuti: www.ibn-tv.com

Vitabu mtandaoni: www.alitrah.info/ebooks/

ISBN 978-998717106-4



9 789987 171064

Cover Design: www.ameerul.com

IMAM HUSAIN (A.S.) NA UWEKAJI MSINGI WA HAKI ZA BINADAMU

